



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

HONG KONG YATOA NAFASI KWA WATANZANIA KUSHIRIKI MAONYESHO YA BIASHARA

Dar es Salaam, 2nd Desemba, 2009: Baraza la maendeleo ya biashara la Hong Kong litakuwa likishikilia idadi kubwa ya maonyesho ya biashara ya kimataifa mwaka 2010 kwa nchi za Afrika ambazo zitapendelea kujiendeleza na kukuza biashara zao.

Akizungumza na vyombo vya habari nchini Mkurugenzi Msaidizi wa HKTDC **Bw. Raymond Yip** alisema nchini mwake kwa mwaka maonyesho zaidi ya 30 hufanyika na kuongeza kuwa katika maonyesho yatakayofanyika January hadi March mwakani wangependa sana wafanyabiashara wa Tanzania zaidi ya 30 kushiriki katika maonyesho hayo.

Aidha **Yip** alitangaza baraza lake kutoa ufadhili wa dola za marekani milioni 10.3 kwa ajili ya kusaidia wafanyabiashara wa afrika kushiriki katika maonyesho nchini humu kuanzia sasa hadi mwezi machi mwakani na kuitaka Tanzania kushiriki.

“Biashara kati ya Tanzania na Hong Kong ni ndogo sana, mwaka jana kati ya nchi hizi mbili ilikuwa yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 49, wakati huohuo uwekezaji ulikuwa dola za kimarekani milioni 8.1” alisema Yip.

Bidhaa za Tanzania zenye kupata soko kubwa nchini kwetu Hong Kong ni pamoja na chai, kahawa, korosho, ngozi, samaki aina ya kamba kochi na vito vya thamani.

Kwa upande wa uwekezaji wa Hong Kong kwa Tanzania, alisema kwanza tunataka mfanye biashara ili wawekezaji waweze kufika hapa kuwekeza kwani uwekezaji ni kama ndoa huwezi kuo pasipo kumpenda mtu.

Tutahakikisha ndani ya miaka mitau tunapata mabadiliko ya kibiashara kati ya Tanzania na Hong Kong tofauti na ilivyo sasa.

“Njooni kufanya biashara Hong Kong watu waliopo huku ni milioni 7 lakini watalii wanaotembelea maonyesho kwa mwaka ni zaidi ya milioni 30 hivyo muone kuwa kuna soko kubwa kwani tuna bandari huru na bidhaa zenu hazitatozwa ushuru zikiingia na malipo yanapatikana hapohapo” alisema Yip.

-Mwisho-